

## MAMLAKA YA MASOKO YA MITAJI NA DHAMANA



### TAHADHARI KWA UMMA

Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA) inapenda kutahadharisha Umma kuwa kuna matangazo ya uwepo wa fursa za uwekezaji danganyifu kupitia mitandao ya kijamii kama WhatsApp, Facebook, Twitter na Instagram zikishawishi Umma kuwekeza katika kampuni na mipango ya uwekezaji wakiahidiwa kupata faida ya asilimia 150% kila siku na kutoa gawio la faida kila baada ya siku 3 kwa kuwekeza kwenye biashara hizo. CMSA inatahadharisha Umma kuwa mipango hiyo ni upatu haramu (pyramid schemes) na wananchi wako katika hatari ya kupoteza fedha zao.

Ikumbukwe kuwa mipango kama hiyo imewahi jitokeza siku za nyuma ikiendeshwa kwa mifumo tofauti tofauti na kusababisha watu wengi kupoteza fedha zao. Mipango hiyo danganyifu inapotosha Umma kuwa ni uwekezaji halali kwa kuweka kivutio cha kupata faida kubwa na kwa haraka. Mifano ya mipango danganyifu ambayo Wananchi walipoteza pesa zao ni pamoja na kampuni ya UPATU, Dollar Jet, Women Empowerment, Development Enterprise Community Initiatives (DECI), na mingine mingi.

Kushiriki katika mipango ya upatu haramu ni kinyume cha Sheria ya Makosa ya Jinai Sura ya 16 ya Sheria za Tanzania, ambapo katika Fungu la 171A, 171B na 171C, ni kosa la jinai kuendesha, kushawishi watu kushiriki, na kushiriki au kuchangia fedha katika upatu haramu (pyramid schemes).

#### **Dalili au Viashiria vya Upatu Haramu**

- Ahadi ya kukuhakishia kupata faida kubwa kwa kipindi kifupi kwa mchango mdogo, bila ya kuwepo na uwezekano wa kupata hasara;
- Hakuna maelezo ya kina ya jinsi faida au fedha zilizoahidiwa zitakavyoweza kupatikana bali huonyesha mseto wa biashara nyingi zisizowiana ili kuvutia mshiriki;
- Mchangiaji hupewa muda mfupi sana kufanya uamuzi wa kujiunga na kwamba endapo hatajiunga mapema atakosa bahati;

- Waendeshaji wana desturi ya kuonyesha kama kivutio kwa wachangiaji wapya orodha ya watu mbali mbali na pengine wenye nyadhifa serikalini, kidini, au katika jamii ambao wameshiriki mpango na kufanikiwa;
- Hakuna mkataba wa kujiunga au kurudishiwa fedha endapo mwendeshaji hatatimiza ahadi zake;
- Hakuna maelezo ya kujitoa katika mpango endapo mshiriki amebadili mawazo ya kuendelea kushiriki;
- Katika mipango hii hakuna mradi maalum wa kuwekeza fedha hizo wala hamna huduma maalumu itokanayo na uwekezaji wa fedha hizo. Mapato ya mpango huo hutokana na wachangiaji wapya na ada ya ushiriki;

Upatu haramu unaendeshwa kwa kutumia kanuni kwamba washiriki wachache wa mwanzo watafaidika na wengi watakaojiunga baadaye watapoteza fedha zao. Vile vile hakuna mfumo ulioandaliwa kwa kuhakikisha kwamba michango yote iliyokusanywa hutumika kwa faida ya wachangiaji.

Mwananchi unashauriwa kutoa taarifa kuhusiana na matangazo, mikutano au mafunzo yanayoendeshwa kushawishi umma kushiriki katika mipango ya upatu haramu. Taarifa kuhusu upatu haramu zitolewe kwa Mamlaka husika ikiwa ni pamoja na Benki Kuu ya Tanzania (BOT), Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA), Kitengo cha Kudhibiti Fedha Haramu (FIU) na vyombo vya usalama - Jeshi la Polisi. Taarifa zitolewe kwa:

**Polisi - Mkurugenzi wa Makosa ya Jinai:** Simu. 0787 668306, 0732 999154.

Tovuti: [www.policeforce.go.tz](http://www.policeforce.go.tz)

Barua pepe: [info.phq@tpf.go.tz](mailto:info.phq@tpf.go.tz)

**Benki Kuu ya Tanzania:** simu (22) 2233000/20

Tovuti: [www.bot.go.tz](http://www.bot.go.tz)

Barua pepe: [adm@bot.go.tz](mailto:adm@bot.go.tz)

**Kitengo cha Kudhibiti Fedha Haramu (FIU):** Simu: 022 2129457

Tovuti: [www.fiu.go.tz](http://www.fiu.go.tz)

Barua pepe: [fiutz@fiu.go.tz](mailto:fiutz@fiu.go.tz)

**Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana:** simu (22) 2114959/61

Tovuti: [www.cmsa.go.tz](http://www.cmsa.go.tz)

Barua pepe: [info@cmsa.go.tz](mailto:info@cmsa.go.tz)

Imetolewa na;

**Afisa Mtendaji Mkuu,**  
**Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana,**  
**Ghorofa ya 6, Jengo la PPF Tower,**  
**Makutano ya Mtaa wa Ohio na Garden,**  
**S.L.P. 75713 Dar es Salaam,**  
**Simu: +255 22 2114959 / 61**  
**Faksi: +255 22 2113846**  
**Barua pepe: [info@cmsa.go.tz](mailto:info@cmsa.go.tz)**  
**Tovuti: [www.cmsa.go.tz](http://www.cmsa.go.tz)**